

## ***Hasara za kutunza vibaya kumbukumbu za shamba***

- ✓ Inapelekea kutokua na uwezo wa kujua kiasi cha fedha kinachoingia na kinachotoka hivyo kutokua na uwezo wa kujua kama unapata faida au hasara.
- ✓ Inapelekea kutokua na uwezo wa kujua vitu vinavyomletea faida au hasara
- ✓ Inapelekea kutokua na uwezo wa kufanya maamuzi sahihi (Manunuzi ya pembejeo, Ubadilishaji wa mazao shambani na uongezaji wa mavuno)
- ✓ Inapelekea kutokua na uwezo wa kutambua ni watu gani unaowadai au wanaokudai na ni kiasi gani.
- ✓ Inapelekea kutokua na uwezo wa kupanga mipango ya kilimo.
- ✓ Inapelekea kutojua nani mteja wako mkubwa na mwenendo wa bei.
- ✓ Inapelekea kutokua na uwezo wa kujua mwenendo wa kilimo chako

**Kwa Maelezo zaidi wasiliana na:**

**Meneja**

**Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania**

**TARI – Kifyulilo,**

**S.L.P 93,**

**Mufindi**

**Iringa - Tanzania.**

**Simu: 0765 1760400769 492549**


**Barua pepe: [cmkifyulilo@tari.go.tz](mailto:cmkifyulilo@tari.go.tz)**

**Tovuti: [www.tari.go.tz](http://www.tari.go.tz)**

**TAASISI YA UTAFITI WA  
KILIMO TANZANIA (TARI)**



**UTUNZAJI KUMBUKUMBU  
ZA SHAMBA**



**“MALI BILA DAFTARI HUPOTEA**

**BILA HABARI”**

## Utangulizi

### *Umuhimu wa kutunza kumbukumbu za shamba*

### *Namna bora ya utunzaji wa kumbukumbu za shamba*

### *Utunzaji kumbukumbu za shamba*

Ni kitendo kinachohusisha uhifadhi taarifa zote zinazohusu kilimo.

### *Aina za Kumbukumbu*

- i. Kumbukumbu za mauzo
- ii. Kumbukumbu za Manunuzi
- iii. Kumbukumbu za vibarua
- iv. Kumbukumbu za ardhi iliyo kodishwa
- v. Kumbukumbu za mali zote zinazomilikiwa na biashara

**Mfano:** Trekta, majembe, godauni, pampu ya dawa n.k

- vi. Kumbukumbu za bili mbalimbali

**Mfano.** Bili za maji, Umeme n.k

- vii. Kumbukumbu za usafiri na gharama zingine.

- a) Inasaidia kujua mzunguko wa fedha (fedha inavyoingia na inavyotoka)
- b) Inasaidia kupanga mipango ya kilimo chako
- c) Inasaidia kupata mikopo katika Taasisi za fedha **Mfano.** Benki, VICOBA n.k
- d) Inasaidia kufanya tathmini ya mwenendo wa kilimo (biashara inakua au haikui)
- e) Inasaidia mkulima kufanya maamuzi sahihi **Mfano:** Maamuzi juu ya kuendelea na kilimo au kuacha
- f) Inasaidia kujua ni wakati gani mauzo ni mengi
- g) Inasaidia kujua ni wakati gani wa kujumua/kununua vitu **Mfano.** Kujua ni wakati gani wa kununua pembejeo za kilimo
- h) Inasaidia kukadiria mapato na kurekebisha matumizi
- i) Inasaidia kutambua changamoto zinazokumba kilimo
- j) Inasaidia kupanga bei ya mazao

- ♣ Tunza kumukumbu zinazofanana kwenye kitabu/ leja/ daftari moja/ ukurasa mmoja.  
**Mfano:** Mauzo yote ya mazao yawekwe kwenye kitabu cha mauzo, manunuzi yote ya pembejeo yawekwe kwenye kitabu/ leja/daftari/ukurasa wa pembejeo n.k
- ♣ Tumia kalamu ya wino (pen) katika kuingiza taarifa kwenye vitabu/leja/daftari. Hii itasaidia kuwa na taarifa za muda mrefu kwani hazitafutika.
- ♣ Weka vitabu/leja/daftari mbali na uchafu, maji, moto, watoto au kitu chochote kinachoweza kuharibu vitabu vya kumbukumbu
- ♣ Weka/hifadhi vitabu/leja/daftari mahali unapoweza kuvifikia kiurahisi. Hii itasaidia kufikia vitabu/leja/daftari pindi unapotaka kuingiza taarifa.
- ♣ Ingiza taarifa kwenye kitabu/leja/daftari kwa wakati, hii itasaidia kutosahau taarifa.

### *Mfano wa Kitabu cha Mauzo ya mazao;*

Tarehe	Jina la mteja	Bidhaa/ zao lililouzwa	Idadi/ kiasi	Bei	Jumla ya Fedha